

Miangwi ya Kimtindo, Kidhamira na Uhusika: Uchunguzi wa Kazi Teule

*Kyallo W. Wamitila*¹

Ikisiri

Makala hii inachunguza namna ambavyo kazi za kifasihi zinaakisi uhusiano na ufanano wa kimatini hasa katika kiwango cha mtindo, dhamira na usawiri na uendelezaji wa wahusika. Msingi wake mkuu ni imani kuwa fasihi inahusiana na fasihi na matini na kazi mbalimbali huingiliana, kuathiriana, kutagusana na kujalizana katika mwanda wa kimwingilianomatini. Matini za kimsingi ambazo zimechunguzwa ni tamthiliya mbili (*Mashetani* ya E. Hussein na *Mashetani Wamerudi* ya S.A. Mohamed), hadithi fupi ya “Mke Wangu” ya M.S. Abdulla na riwaya ya *Wenye Meno* ya S.A. Mohamed, zilizoteuliwa kimakusudi. Uchunguzi huo umefanywa kwa kuzingatia mawazo ya Nadharia ya Mwingilianomatini inayohusishwa na Julia Kristeva aliyebuni dhana hii mwaka 1966. Kristeva aliyakuza mawazo yake kwenye msingi wa dhana ya usemezano inayohusishwa na mwanaisimu, mwanafasihi na mwanafalsafa wa Kirusi, Mikhail Mikhailovich Bakhtin. Makala hii imebainisha sifa na viwango mbalimbali vya udhihirikaji huo wa mwingiliano na kuzungumzia athari zake katika uendelezaji wa maana ya kifasihi na fasiri za kifasihi zinazofuatia.

1.0 Utangulizi

Katika historia ya nadharia ya fasihi, uhusiano baina ya matini au kazi za kifasihi ulichunguzwa kwa kurejelea dhana ya 'kuathiriwa'. Hata hivyo, dhana hii ya kuathiriwa iliishia kupuuzwa. Katika miaka ya karibuni, uhusiano huo unazungumziwa na kuchunguzwa chini ya dhana ya 'mwingilianomatini'. Dhana hii inahusishwa kwa kiasi kikubwa na Julia Kristeva (ambaye aliitegemeza kwenye dhana ya Mikhail Bakhtin ya usemezano). Baadhi ya wananadharia kama Julia Kristeva, Roland Barthes na Jacques Derrida wanaamini kuwa mwingilianomatini ni sifa bia ya matini. Wengine kama vile Linda Hutcheon (2002) wanaieleza hii kama sifa ya kimsingi ya umatini.

Kimsingi, mwingilianomatini unachunguza 'maada' inayoingia kwenye matini nyingine na kubainisha ni lipi hasa linalotokea kwa maada hiyo: inavyobadilishwa, kugeuzwa, kufinyangwa, na kuhulutishwa katika matini hiyo

¹ Profesa Mshiriki, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya. Barua pepe: wamitila@gmail.com

mpya. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa maada hiyo inayoingia kwenye matini inadhibitiwa na kanuni za matini mpya. Hapa ina maana kuwa pana haja ya kuiwazia maada hiyo katika muktadha wa utambulisho wa matini mpya (yaani inajibainisha kibinafsi kama matini maalumu).

Katika sehemu ifuatayo, tutaangalia mwingilianomatini kati ya kazi nne zifuatazo: *Mashetani* (E. Hussein) na *Mashetani Wamerudi* (S. A. Mohamed) na hadithi fupi ya “Mke Wangu” (M. S. Abdulla) na riwaya ya *Wenye Meno* (S. A. Mohamed). Uteuzi wa kazi hizi ni wa kimakusudi kwa kuzingatia jinsi kazi zinavyoakisi sifa tofautitofauti za mwingilianomatini.

2.0 Mashetani ya E. Hussein na Mashetani Wamerudi ya S. A. Mohamed

Tofauti na kazi nyingi za kimwingilianomatini ambapo msomaji anaishia kugundua na kubainisha uhusiano wa kimatini, tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* inamwelekeza msomaji kwenye mwingilianomatini huo katika kiwango ambacho wana-naratolojia watakieleza kama cha kipara-matini; kwanza, katika kichwa chenyewe, na pili, katika dibaji ambapo mwandishi haelekezi kwenye sifa hiyo ya mwingilianomatini tu bali ‘anaumuktadhisha’ mwingilianomatini wenyewe katika fasihi ya Kiswahili kwa kurejelea kazi nyingine chache ambazo, kwa maoni yake, zina sifa hiyohiyo. Dibaji hii ni kile ambacho Gerard Genette katika *Paratexts* anakieleza kama paramatini ya mwandishi. Ni dibaji ambayo, kama anavyoeleza Genette, inatuelekeza kwenye 'lengo au dhamira ya mwandishi' na, kwa kiasi fulani, kwenye hali ya mwandishi kuelekea kudhibiti (au kujaribu kufanya hivyo) maana ya matini. Kimsingi, hii ni kazi ambayo inaelekeza jinsi inavyotaka isomwe. Genette anadokeza kuwa tatizo kuu la dibaji ni kuwa inakuwa aina fulani ya hali ya mawasiliano yenye msingi unaotetereka hasa kwa kuwa mwandishi anawasilisha kwa msomaji 'tahakiki ya mapema ya matini ambayo bado (msomaji) hajaikabili.' (1997: 237).

Hata hivyo, msomaji ambaye anaelewa fasihi ya Kiswahili huenda asielekezwe na paramatini hiyo bali na kichwa cha kitabu chenyewe hasa kwa kuzingatia kuwa tamthiliya ya *Mashetani* ya E. Hussein, ambayo ni matini-tangulizi yake, ni mojawapo wa kazi kuu katika fasihi ya Kiswahili.

Tamthiliya ya Said A. Mohamed inayaibua masuala mengi ambayo yatamshughulisha msomaji na mhakiki makinifu wa kazi hii. Kwanza, kinyume na *Mashetani* ya E. Hussein ambayo inaelekea kuashiria kuwa 'mashetani' (ishara ya wakoloni na mfumo wa ubepari) hawakuondoka barani Afrika au katika mataifa yaliyotawaliwa bali walichokifanya ni kuabadili mfumo wao wa kiunyonyaji, *Mashetani Wamerudi* inasema kuwa 'wamerudi'. Hapa pana uelekezi mkubwa kwenye kurejelea katika hali ya moja kwa moja (yaani kwa utawala wa kiuwakala unaoelekea kudokezwa katika *Mashetani*). Dhana ya kurudi inaweza pia kufasiriwa kama usomaji au ufasiri kombo wa kidhamira wa *Mashetani* (kuchukuliwa kuwa inaashiria kuwa walishaondoka). Matini ya ndani au kimatini kilichoko kwenye kichwa hiki ni kuwa ukoloni mpya umeanza kupitia mfumo wa

utandawazi au ubepari wa kiutandawazi unaoshamiri ulimwenguni kwa sasa, na labda kwa mkondo na mfumo ambao una matokeo hasi kwa mataifa yetu. Pili, 'wamerudi' hapa ni uchimuzi ambao mwandishi anataka ubakie katika akili ya msomaji kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Katika muktadha huu, kwa mtazamo wa Michel Foucault, hapakuwako na mkatiko wa ki-epistemolojia (kuhusu maarifa ya ukoloni) uliowahi kufanyika bali mfumo wenyewe umekuwako tangu hapo isipokuwa kwa mgeuko wa ki-istilahi au kimaneno tu. Katika ulumbi au usemi wa kila siku, tunaona mabadiliko haya kutoka 'mkoloni', 'mfadhili' hadi 'mshirika kwa kimaendeleo'. Kwa msingi huohuo wa ki-Foucault, tunaweza kusema kuwa kurudi huku kwa 'mashetani' kunakoashiriwa katika tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni dhahirisho la upofu wa 'epistimu' ulioshamiri baada ya ukoloni mkongwe kuondoka kuhusu hatima ya mataifa ya Kiafrika na raia wake.

Tamthiliya ya *Mashetani* ya E. Hussein inaangalia suala la ukoloni na ukoloni mamboleo kupitia marafiki wawili, Juma na Kitaru, na inabakia kuwa mojawapo ya tamthiliya bora za baadaukoloni. Juma anatokana na jamaa ambayo ilikuwa katika tabaka la juu (la mamwinyi) kabla ya majilio ya uhuru ilhali Kitaru anawakilisha tabaka ambalo limenufaika kutokana na mabadiliko hayo. Tamthiliya hii imemuktadhiswa kwenye historia ya Unguja (ambapo kuna mabadiliko yaliyofanyika na kuuangusha mfumo wa mamwinyi). Uhusiano wao kama marafiki unakabiliwa na mvutano huo wa kitabaka ambao unatishia kuuharibu uhusiano wao. Jamaa ya Juma (ikiongozwa na bibi yake) inatamani kuyakwamiza mawazo yake kwenye ukale au jana yao. Yamkini sifa hii inatokana na uhalisi kuwa hali ya maisha ya jamaa hiyo leo yao ni mbaya. Huu ni mkabala ambao unatukumbusha mitazamo ya kisaikolojia. Jana inakuwa kama pahali pa kukimbilia ili kuepuka kukabiliana na leo.

Kitaru anauona ugumu wa kujitambulisha na jamaa yake na hasa babake ambaye ndiye kielelezo kikuu cha uroho na umero wa tabaka jipya ambalo linatamani kujilimbikizia utajiri kama njia ya kuifuta jana yake. Huenda hamu hiyo ya utajiri inaongozwa na hofu ya jana (walipokuwa maskini) ikiwa tutaiangalia tamthiliya hii kwenye mkumbo huohuo wa kisaikolojia.

Katika tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*, kiini cha matendo ya tamthiliya ni Profesa. Mhusika huyu anaweza kuangaliwa kuwa aina fulani ya mhusika mchomozi anayefasiri matukio mengi katika ulimwengu wa tamthiliya hii. Aidha, anaweza kuangaliwa kama sitiari ya nafsi ya umaizi na ung'amuzi ambayo ni muhimu katika kuielewa jamii ya leo ya utandawazi.

2.1 Urejelezi wa Ishara

Mojawapo wa sifa anayoitambua msomaji wa *Mashetani Wamerudi* ni kuwapo kwa ishara ambazo zinaihusisha au kuifungamanisha moja kwa moja na tamthiliya ya E. Hussein. Ishara hizi ni 'mbuyu', 'upepo', 'shetani', 'mbuyu', 'waltz', 'ngazi', n.k. Baadhi ya ishara hizi zinaelekea kujenga uhusiano wa moja kwa moja kwa

kuwapo na muunganiko wa kidhamira. Hata hivyo, ishara nyingine zinaishia kutumiwa kwa namna ambayo inaweza kuangaliwa kama namna ya kuupanua msingi wake au kwa aina fulani ya uundajiupya wa kiubunifu.

Katika *Mashetani* ishara za 'Binadamu' na 'Shetani' zinawasilishwa kwa namna ambayo msomaji anapewa au anaachiwa kazi ya kifasiri ili kuweza kutambua zinarejelea na kuashiria nani. Katika *Mashetani Wamerudi*, ugumu au utata huo wa kiishara haupo. Hii haitokani na kuwapo kwa uhusiano wa kimwingilianomatini tu (ambao unaweza kumwelekeza msomaji kwenye maana au fasiri zinazotokana na tamthiliya ya E. Hussein) bali na kwamba tamthiliya hii ya *Mashetani Wamerudi* imefasiri hilo mara kadhaa kupitia kwa mhusika wa kikorasi, Mwanambebe. Pia, hilo linajitokeza katika mazungumzo ya wahusika mbalimbali na maelekezo ya jukwaani ambayo kwa kiasi kikubwa yanaelekea kuchimuza mno sifa ya kisimulizi katika tamthiliya hii. Msomaji wa *Mashetani Wamerudi* ataelekea kutambua 'virejelewa' vya ishara za 'Binadamu' na 'Shetani' kwa wepesi zaidi kuliko msomaji wa *Mashetani*.

Ishara ya 'mbuyu' ni muhimu sana katika tamthiliya zote mbili. Katika *Mashetani*, mbuyu unaweza kuangaliwa kama ishara ya nchi na chimbuko la wanajamii. Hii ni ishara ambayo inafungamana kwa kiasi kikubwa na utamaduni wa jamii inayozungumziwa. Inawezekana kusema kuwa maana hii inaendelezwa kwenye tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ingawa inawezekana pia kudai kuwa katika tamthiliya hii mbuyu unapoteza ile kani yake ya *Mashetani* na kuishia kuwa nguzo ya kimandhari tu. Pili, kuwapo kwa mfumo wa kiutandawazi kunaelekea kuidengua misingi ya kitamaduni ya kuutazama mbuyu na labda kwa jinsi hii kuelekeza kwenye sifa za umahuluti wa kitamaduni unaozungumziwa na wahakiki kama Homi Bhabha.

2.2 Uhusika na Mwingilianomatini

Katika sehemu iliyotangulia tumedokeza kuwa pana uhusiano wa kihusika kati ya tamthiliya hizi mbili. Msingi mkuu wa uhusika ni jira ya kilinganuzi ya 'Binadamu' na 'Shetani'. Kimsingi, mhusika 'Shetani' anaweza kuangaliwa kama ishara ya 'mkoloni' au picha zake tofauti katika mpito wa wakati. Hata hivyo, katika tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*, mhusika 'Shetani' anawasilishwa kama 'Sheta'. Kifupisho hiki cha jina kinaweza kuangaliwa kwa namna mbalimbali. Kwanza, kama mbinu anayoitumia mtunzi kumpa mhusika huu utambulisho wake ambao, kwa kiasi fulani, unajitofautisha kwa namna fulani na mhusika Shetani wa *Mashetani* na wakati huohuo kuujenga uhusiano. Pili, uhusiano uliopo kati ya mataifa yanayoendelea na yale yanayoongoza mfumo wa ubepari wa kimataifa (utandawazi) umejengwa katika usemi unaowapumbaza watawaliwa kuhisi kuwa wana uhusiano wa karibu na wakoloni wa siku hizi. Yamkini uhusiano huu ndio unaofumbwa na jina 'Sheta' ambalo linaondoa mipaka na umbali kati ya makundi mawili.

Tatu, jina hili linaweza kuangaliwa na kufasiriwa kwa namna nyingine. Kiswahili kina neno 'sheta' ambalo huweza kutumiwa kwa maana ya 'kandamiza' 'ponda' au 'vuruga'. Fasiri hii inalifanya jina lenyewe kuwa ishara muhimu ya ki-onomastiki au kimajazi kuuelezea wasifu unaohusishwa na mataifa yanayoongoza na kushikilia hatamu za utandawazi. Kwa msingi huu, linaishia kuwa na uashiriaji mara mbili linapolinganishwa na Shetani lililotumiwa na E. Hussein katika tamthiliya yake.

Wahusika wengine ambao wanaelekea kuhusiana ni 'Kitaru' na 'Juma' katika *Mashetani* na 'Jumai' na 'Kitarua' katika *Mashetani Wamerudi*. Kisa cha wahusika hawa kinaelekea kuibua masuala kadhaa. Sifa ya kwanza ambayo inabainika ni majina yao ambayo yanaendelezwa tofauti (kwa kuongezwa kwa herufi moja kwenye majina yao). Yamkini suala la kubadilisha majina linaweza kuangaliwa kama njia mojawapo anayoitumia mwandishi kuwapa utambulisho tofauti kama tulivyooona hapo nyuma. Hata hivyo, tunaweza pia kuiangalia sifa hii kwa kuirejelea dhana ya 'tessera' inayozungumziwa na mhakiki Harold Bloom katika kitabu chake *The Anxiety of Influence*. Bloom anaitumia dhana hii kuelezea hali ambapo mwandishi 'anaendeleza au kukamilisha' kazi/matini au kitu (au katika muktadha wetu mhusika kwa namna fulani ya kiulinganuzi- kinyume na ilivyo katika matini tangulizi.

Hata hivyo, uhusika wa wahusika hawa katika *Mashetani Wamerudi* si mpana na labda sifa ya kilinganuzi inaweza tu kuhusishwa na Kitarua. Katika tamthiliya hii, Mzee Kitarua anahusishwa na tabaka lililotwaa mamlaka/uongozi baada ya ukoloni mkongwe kuondoka. Kijuujuu, tunaweza kusema kuwa hii ni sifa inayomhusisha na Kitaru katika tamthiliya ya *Mashetani*. Hata hivyo, tofauti inazuka tunapowatathmini wahusika hawa wawili kwa undani. Katika *Mashetani*, jamaa ya Kitaru inahusishwa na tabaka hilo na babake hasa ndiye ishara kuu ya tabaka lenyewe. Kitaru, mhusika anayejikuta njiapanda, ni mtoto wa mtu aliyeko katika tabaka la juu na anayeona fahari kujitambulisha na tabaka hilo. Kitaru angetamani kujinasua na kujitenga na uhalisi huo (jambo ambalo linaashiriwa na ile ndoto anayoiota anapoota akiota manyoya naye akijaribu kuyanyonyoa kila yanapoota. Hata hivyo, katika *Mashetani Wamerudi*, Mzee Kitarua anajitambulisha moja kwa moja na tabaka hilo na hata kujuta kwa sifa hiyo. Tunasoma:

Mzee Kitarua: Kwa sababu hiyo ndiyo maana mimi na Jumai tumekuja kukuhakikishia kwamba mfarakano baina yetu haupo tena. Mimi nimeshafunzwa na ulimwengu. Nimeshaufahamu mfumo uliopo wa kujijazia mali, bila ya kujali wananchi wenzetu. Nimeshazungumza mara nyingi na wewe Prof. kuwa mfumo huu wa uchumi na jamii ni mfumo wa kupanda na kushuka,
(Mohamed, 2016: 64-5).

Mtazamo wa kitabaka na tofauti za kitabaka katika *Mashetani* zinapitia mabadiliko na hili ni suala ambalo linatuelekeza kwenye mawazo ya mwananadharia wa ubaadaukoloni, Stuart Hall, kuhusu utambulisho kutokuwa katika hali funge bali kuwapo katika aina ya mchakato na mageuzi ya kudumu. Tukirejelea katika tamthiliya ya Hussein, tunaikumbuka ishara ya ‘manyoya’ katika ndoto anayoiota Kitaru. Anaota akiota manyoya ambayo anajaribu kuyanyonyoa lakini kila anapofanya hivyo, manyoya hayo yanaota tena. Tunasoma:

Mimi. nakumbuka, nikaanza kuwa na hofu. Nikaanza kunyonyoa manyoya yangu. Lakini kila nikijinyonyoa, mengine yanaota. Yananiziba pumzi. Mengine yanaota, makubwa zaidi na yenye nguvu zaidi kuliko yale. Nikaanza kuingiwa na shaka (Hussein, 1973: 49).

Kwa misingi ya mawazo ya Harold Bloom, inawezekana kudai kinachofanyika katika *Mashetani Wamerudi* ni ukamilishaji wa kitanakuzi. Mwandishi anafanya hivi kwa kuonesha taswira ya kinyume—na kwa namna hiyo kuikwepa ile hofu ya kuathiriwa anayoizungumzia Bloom katika andiko lake. Kwa upande mwingine, inawezekana kuiangalia hali hii, kwa misingi ya mawazo hayohayo ya Harold Bloom, kwa kuirejelea dhana yake nyingine anayoiita 'klinameni'. Hii ni dhana ambayo inatokana na Kiyunani na ilitumiwa katika fani ya sayansi kuelezea mgeuko wa ghafla wa atomu. Bloom anaitumia dhana hii kurejelea: mwelekeo wa matini kuisoma kombo matini au, kwa kutumia dhana yake nyingine, upitiajiupya wa matini iliyotangulia. Kwa upande mwingine, inawezekana mchezo wa 'mashetani' anaoutaka Kitaru waucheze na Juma katika sehemu ya mwisho ya *Mashetani* (na hasa kwa kutaka kuicheza nafasi ya Shetani) unaweza kuruhusu fasiri hii.

Bloom anauangalia uhusiano uliopo baina ya mwandishi na mwandishi-mtakadamu/mtangulizi wake kama ule uliopo baina ya mtoto wa kiume na babake katika misingi ya mawazo au saikolojia ya Freud. Uhusiano huo unatawaliwa na sifa mbili kuu: mapenzi na ushindani. Kwa mujibu wa Bloom, uhusiano wa waandishi hao basi ni wa ki-Edipode. Katika kisasili cha Edipode, tutakumbuka kuwa Edipode aliishia kumuua babake. Hata hivyo, 'kifo' kinachorejelewa hapa ni cha kiishara na hutokea kwa aina fulani ya upitiajiupya wa matini ya mwandishi aliyetangulia au usomajikombo wa matini hiyohiyo. Anachofanya mwandishi mpya ni 'tendo la usahihishaji wa kibunifu ambao kimsingi ni fasirikombo' (Bloom, 1975: 30).

Tunapouchunguza usawiri wa Mzee Kitarua tunaweza kueleza kwa dhana kadhaa za Bloom. Kwanza, kuna hiyo klinameni (usomaji kombo). Pili, unaweza kuangaliwa kwa misingi ya mkakati au mbinu ya mtenganiko au kenosisi - ambapo pana mwelekeo wa kuwako na utengano na tofauti kati yake na mhusika wa matini-tangulizi. Kwa msingi huu, inawezekana kudai kuwa usomaji wa aina hii ni wa kimakusudi na kwa hiyo sehemu ya utambulisho wa mhusika mpya au ni hali ya usemezano kwenye misingi ya mgongano wa kimtazamo. Pia, kuna jinsi au

namna nyingine ya kuliangalia jina la Kitarua. Tunaweza kuiangalia kama tamathali ya usemi inayojulikana kama 'metaplasumus' au tutakayoiita hapa 'hijakombo' - ambapo uendelezaji wa neno unafanywa kombo kimakusudi.

2.3 Miangwi ya Kidhamira na Suala la Upanuzi wa Kimuktadha

Tamthiliya hizi mbili zinahusiana kwa kuangalia suala la uhusiano kati ya mataifa huru na mataifa ya kikoloni. Tamthiliya ya *Mashetani* inajifunga kwenye uhusiano huo baina ya mataifa yaliyotawaliwa na wakoloni na uhusiano baada ya ukoloni mkongwe kuondoka na kuendelea kutawala kwa mfumo wa ukoloni mamboleo kupitia mfumo wa kiuwakala wa ukoloni - ambapo tabaka lililochukua madaraka linaendeleza mfumo wa utawala unaoendeleza mifumo ya kiunyonyaji iliyokuwako. Kwa upande wake, *Mashetani Wamerudi* inaendeleza dhamira hii kwa kuangalia jinsi mfumo huo unavyokuzwa katika mfumo wa utandawazi ambao, kimsingi ni ubepari wa kifedha. Tamthiliya hii inahoji mifumo hiyo, itikadi ya kih hegemonia inayotawala pamoja kuidengua simulizi kuu ya ukoloni.

Suala hili la simulizi kuu linatokeza mara kadha kupitia mhusika wa kikorasi, Mwanambele. Tunasoma:

Mwanambele: Sauti kubwa ya kujenga ubwana,
Wakati uliopita na uliopo,
sauti ya u-masta, sauti ya ubwana,
Lakini sasa ubwana unapigwa teke,
Lazima tuupige teke ubwana
Teke la 'grand narratives'.... (Mohamed, 2016: 15)

Inahalisi kukumbuka kuwa uhusiano uliokuwako/ulioko baina ya mataifa ya kikoloni na makoloni yao (au mataifa huru) umejengwa kwenye 'simulizi kuu' ya kibeberu. Lengo la simulizi hii ni kumsawiri mtawaliwa kama Wingine. Huyu ni kiumbe ambaye hana uwezo wowote na ambaye anajikuta katika mazingira ambayo nayo yana mchango katika hali yake. Mtawaliwa wa aina hii anasawiriwa kama anayeishi kwenye utupu au uwazi fulani wa kitamaduni, yaani kama kiumbe, hana jinsi yoyote ya kujielezea kiutamadani. Uwazi au utupu huo wa kiutamaduni ndio ambao mkoloni (au mataifa yanayoshika hatamu za utandawazi yanapania kujaliza. Hii inamaanisha kwamba, mtazamo uliopo unaelekea kumwangalia na kumsawiri mtawaliwa kama asiyekuwako na ambaye anapaswa kughoshiwa na utamaduni wa kibeberu.

Katika tamthiliya ya *Mashetani*, mojawapo ya ishara kuu ya mwelekeo huo wa kujaliza pengo hilo la kitamaduni ni ile ya 'waltz' ambayo ni aina ya ngoma ya Ulaya inayochezwa na watu wawili walioshikana kwa karibu sana. Kimsingi, tunaweza kusema kuwa suala la utamaduni na mtazamo wa mkoloni kumhusu mtawaliwa linaibushwa katika tamthiliya ya *Mashetani* na labda kusesitizwa zaidi katika *Mashetani Wamerudi* sio tu katika mazungumzo (kupitia maneno ya Prof.,

Kijana 1, Kijana 2, Mzee Kitarua, Mzee Jumai, na hata ya umati) bali pia kupitia kwa mhusika Mwanambebe ambaye anapewa jukumu la kimeta-tathmini (kutoa tathmini au maoni kuhusu matini yenyewe).

Sifa hii iliyozungumziwa hapo juu inaifanya tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* kuwa na sifa ya usimbaji mkubwa wa kiitikadi na kinadharia ikilinganishwa na *Mashetani* ambayo uwasilishaji wake wa kidhamira umejengwa na kuimarishwa zaidi na uchangamano wa kiishara na lugha ya kitamathali.

Tamthiliya ya *Mashetani* imejengwa kwenye muktadha wa kiurejelezi wa nchi za Kiafrika. Hata hivyo, inawezekana kudai kuwa mkabala wake wa kidhamira haujifungi kwenye Afrika tu. Fasiri ya aina hii inaelekea kuwa ya kijumla kwa kuwa pana suala la uhusiano baina ya mkoloni na mtawaliwa (wakati wa enzi ya ukoloni na ile ya ukoloni mamboleo) hali iliyotokea kwingineko. Kwa upande wake, mhusika wa kikorasi, Mwanambebe, anabainisha waziwazi kuwa muktadha wa kiurejelezi wa *Mashetani Wamerudi* ni mpana zaidi. Aidha, dhamira ya utandawazi au ubepari wa kifedha na matokeo yake ulimwenguni inatukumbusha upana huo wa kimtazamo.

2.4 Ukoloni, Ukolonimamboleo na Utandawazi

Dhamira ni msingi muhimu wa mwingilianomatini wa kazi hizi mbili. Jira kuu ya mwingilianomatini huo ni uhusiano baina ya mkoloni (kwa upande mmoja) na Wingine (kwa upande wa pili) - binadamu, mtawaliwa au mataifa ya baadaukoloni. Uhusiano huo umejengwa kwenye misingi ya unyonyaji na ukandamizaji. Msingi wa unyonyaji huo ni imani ya 'uwezo wa kiukombozi' waliojipa wakoloni ambao ulikuwa msingi wa kuimarishwa kwa madai yaliyodhamiriwa kuuhalalisha utawala wa kidhalimu au kinachoelezwa kama simulizi kuu. Katika tamthiliya ya *Mashetani*, kuna sitiari na ishara muhimu ya Chewa ambayo inafumbata sifa ya kidhamira ambayo kwa kiasi fulani inaakisiwa na *Mashetani Wamerudi* japo haikurudiwa. Tunasoma:

Kitaru: Hadithi ya chewa. Mbali sana, ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa.
Chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia
kinywani mwake. Anaweza kutoka aliko, kuivuta na kuimeza mashua
yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji, ikitaka
isitake. Na huyu chewa siyo chewa bali ni shetani
(Hussein, 1973: 28).

Katika tamthiliya hii, taswira hii ya kiishara inaelekeza kwenye uwezo wa nguvu za kikoloni kuendeleza ukandamizaji na mfumo wake kupitia mfumo wa ukoloni mamboleo ambapo hapana lazima ya mkoloni mwenyewe kuwapo mahali ili kuuendeleza unyonyaji wake. Hii ni ishara ambayo, kwa namna fulani, inaakisiwa au kupigiwa mwangwi katika *Mashetani Wamerudi* ambapo mfumo wa aina hii unaendelezwa kupitia utandawazi.

2.5 Mwanda - Mandhari na Wakati

Medani muhimu ya mwingilianomatini ya kazi hizi mbili ni mwanda. *Mashetani* inajihusisha na kipindi cha kihistoria kinachofuatia baada ya kuondoka kwa ukoloni mkongwe na kuimarika kwa ukoloni mamboleo. *Mashetani Wamerudi*, kwa upande wake, inashughulika na muktadha wa baadaukoloni (na kwa kiasi fulani inaweza kuangaliwa kama inayoendeleza wakati unaoashiriwa katika tamthiliya ya E. Hussein). Kwa kiasi kikubwa, tunaweza kusema kuwa mwanda wake ni mpana kuliko ule wa *Mashetani*.

Suala la upana wa mwanda halikomei tu kwenye mandhari ya kiwakati bali pia mwanda wa kijiografia. Hii ni tamthiliya ambayo inashughulika na dhamira za baadaukoloni. Ingawa kimsingi, muktadha wake wa karibu ni taifa au mataifa ya Kiafrika, pana uelekezi bayana ambao unaiweka tamthiliya hii kwenye muktadha mpana (tunaweza kurejelea kauli za Mwanambebe). Hali hii inaifanya tamthiliya hii kuwa aina fulani ya mlumbo au diskosi ya kipinzani (dhidi ya diskosi ya kihegemonia inayohusishwa na utandawazi).

2.6 Wahusika na Mwanda wa Kimwingilianomatini

Kiwango cha kimsingi cha uhusiano baina ya wahusika, kama tulivyoona hapo juu, kipo kwenye uteuzi wa majina na shaksiya za utambulisho alizonazo mhusika au walizonazo wahusika mbalimbali. Katika tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*, tuliona sifa hii kutokana na kuwapo kwa majina yanayokaribiana (Shetani katika *Mashetani* na Sheta katika *Mashetani Wamerudi*). Aidha, kuna tofauti ndogo zinazotokea katika majina na ambazo hazifichi uhusiano huo kabisa. Hapa tunaweza kurejelea wahusika Kitaru na Juma ambao wanawasilishwa kama Mzee Kitarua na Mzee Jumai katika *Mashetani Wamerudi* kama njia ya kuashiria na kufumbata mpito wa wakati (hasa kwa kuwepo na neno 'Mzee').

Kwa kuhitimisha sehemu hii, mwingilianomatini unabainika katika kiwango cha kidhamira, kimtindo na kisemiotiki katika kazi zinazohusika kwa namna isiyoepukika na jicho la msomaji.

3.0 Mihusianisho ya Kimwigo na Ubunifu: “Mke Wangu” ya M. S. Abdulla na Wenye Meno ya S. A. Mohamed

Neno 'mhusianisho' (wingi: mihusianisho) limetumiwa hapa kwa maana ya sifa ya kazi au matini kujihusisha kwa urejelezi na kazi au matini nyingine iliyoitangulia. Kazi ambazo zinachunguzwa hapa zinatofautiana na kazi zilizotangulia kiutanzu. Kazi zilizozungumziwa hapo juu ni za kidrama (yaani zipo kwenye utanzu mmoja). Matini zinazochunguzwa hapa zipo kwenye tanzu tofauti. Moja ni hadithi fupi (“Mke Wangu”) na nyingine ni riwaya (*Wenye Meno*).

Uhusiano uliopo baina ya kazi hizi mbili ni, kwa kiwango cha juujuu, kama uliopo baina ya tamthiliya ya E. Mbogo, *Giza Limeingia*, na riwaya ya Mbunda

Msokile, *Usiku Utakapokwisha*, ambapo kazi iliyoko kwenye utanzu mmoja inawasilishwa katika utanzu mwingine (na kuishia kudumisha kwa kiasi kikubwa sifa za matini tangulizi). Msingi huu wa utanzu una athari fulani katika suala zima la mwingilianomatini.

Riwaya haina ubanifu ulioko kwenye hadithi fupi. Upana wa utanzu huu unamwezesha mwandishi kuuchukua mkabala tofauti kuhusu mawanda ya ulimwengu wa kibunilizi-mandhari, suala la wakati, mtazamo, kina cha kidhamira, na uhusika. Hata hivyo, misingi ya mwingilianomatini inabakia palepale. Uchunguzi wa ndani wa riwaya hii ya *Wenye Meno*, umebainisha kuwa tofauti na *Usiku Utakapokwisha* ambayo kimsingi inairudia hadithi ya *Giza Limeingia*, riwaya ya S. A. Mohamed inaandika upya hadithi ya “Mke Wangu” ambayo inatukumbusha riwaya ya mwandishi wa Peru na mshindi wa Tuzo ya Nobel, Mario Vargas Llosa ya *The Bad Girl* inapolinganishwa na *Madame Bovary* ya G. Flaubert.

3.1 Msuko kama Nguzo ya Mwingilianomatini

Katika hadithi ya “Mke Wangu”, msimulizi anaeleza jinsi alivyoishia kumwoa Aziza. Aliwakataa wachumba wote aliopendekezewa na wazazi wake kwa sababu tofautitofauti: Fedhele Salimu kutokana na tabia yake ya kuzurura usiku na marafiki zake; Salma kutokana na tabia yake ya kutumia rangi mashavuni na midomoni, na Seluwa kwa kuwa na kidomo. Hatimaye, msimulizi anamwoa Aziza, msichana wa shamba na ambaye anamwona kama asiyeweza kuwa na tabia za wasichana wa mjini (na ambaye anatamani kumpevusha). Hata hivyo, pana tofauti kubwa ya kimtazamo kati ya wahusika hawa wawili kuyahusu maisha.

Maisha ya ndoa kati ya msimulizi na Aziza yanakumbwa na matatizo mengi tu. Aziza hapendezwi na tabia ya mumewe ya kutofanya kazi na kuendelea kuwategemea wazazi wake. Aziza anashindwa kuelewa kwa nini mumewe analalamika kuwa hapati kazi japo kuna kazi nyingi (k.v. kuangua nazi, kuchunga punda au kuchoma mihogo). Aziza analalamika kuihusu mikono laini ya mumewe ambayo, kwa maoni yake, si mikono ya mwanamume. Aziza mwenyewe hakubali kufuliwa nguo na mfanyakazi na wala haoni sababu ya kuvaa viatu au hata kupiga mswaki kwa mtindo wa kisasa.

Tunamwona Aziza, hatimaye, akivutiwa na muuza madafu ambaye anamwona kama kielelezo cha mwanamume anayefanya kazi au kujitahidi na ambaye ni kufu yake. Hadithi inapoisha Aziza ambaye amechoshwa na tabia yake hiyo anataka talaka ili aolewe na muuza madafu ambaye ni kufu yake na licha ya kuwa wa tabaka tofauti, anampenda (na muhimu zaidi) anafanya kazi badala ya kuwategemea wengine.

Msuko huu unaakisiwa kwa kiwango fulani na hadithi ya riwaya ya *Wenye Meno*. Hata hivyo, pana tofauti moja ya kimsingi: mkabala wa kisimulizi. Hapa pana Halima, ambaye alitoroka nyumbani mamake mzazi alipotaka kumwoza kwa mwanamume asiyempenda. Halima, tofauti na Aziza, ni mwanamke msomi na

mtemedeni ambaye anaishi katika ulimwengu wa leo unaohimiza na kusisitiza umuhimu wa haki za wanawake na uhuru walio nao wa kujiamulia mambo yanayohusiana na maisha yao. Halima anaandamwa na mwanamume tajiri ambaye anamtamani na ambaye anautumia utajiri wake kujaribu kumnasa lakini naye anajikwamua kwenye mitego yake hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa inaendeleza na kuakisi tandabui za ubabedume na mtazamo dhalilishi kwa mwanamke. Hatimaye, kama Aziza wa Abdulla, Halima naye anaishia kumtamani Sudi (ambaye anajulikana kwa jina la majazi la Muuza Madafu). Mfanano huu hauishii kwenye mhusianisho wa kihusika bali unaelekea kutokeza kwenye kiwango cha umotishaji.

Utanzu wa hadithi fupi unamnyima mwandishi wake nafasi ya kueleza kwa tafsiri uhamasishaji wa matendo. Hali hii inatokeza katika riwaya ya *Wenye Meno*, kwa sababu jinsi Halima anavyoishia kumpenda Muuza Madafu inakosa uhamasishaji bayana na kwa kiasi kikubwa inaishia kuwa na uchocheaji wa nje kutokana na matini-tangulizi au matini-chanzi yake. Hali hii inaweza kuhusishwa na uhalisi kuwa mkazo mkubwa upo kwenye kuwa kwake kama mhusika mchomozi. Huyu ni mhusika anayefasiri na kuufafanua ulimwengu wake zaidi ya mengine; na kwa kiasi fulani kumfanya awe kama mhusika anayechukua mkabala wa 'mhusika-mhakiki' wa ulimwengu wake wa kibunilizi.

Suala jingine muhimu ni kuwa *Wenye Meno*, ni hadithi pana na changamano ambayo haijifungi tu kwenye suala la mapenzi na ndoa bali inaliangalia suala zima la uhusiano wa kitabaka katika viwango tofautitofauti na kani za kiuchumi/kibepari katika ulimwengu wa leo.

3.2 Uhamasishaji na Mhusika: Utata wa Mwingilianomatini wa Kihusika

Katika sehemu iliyotangulia, tumeona jinsi ambavyo wahusika Aziza na Halima wanaingiliana. Uhusiano wao huo hauishii kwenye namna wanavyoishia na 'Muuza Madafu' (japo katika *Wenye Meno* 'muuza madafu' huyo kapewa (ma)jina-Mustaffa/Sudi). Pana kiwango kingine cha mwingilianomatini huo - kile cha uhamasishaji au umotishaji. Katika hadithi fupi ya "Mke Wangu", Aziza anampenda muuza madafu kwa kuwa 'ni kufu yake' tofauti na mumewe, huyu anafanya kazi kwa mikono yake na wala hategemei mtu mwingine. Katika *Wenye Meno*, msingi huo wa kutenda kazi labda si muhimu (madhali 'Mwenye Meno' anayo kazi na anazo pesa).

Halima ni mhusika ambaye ana uwezo mkubwa wa kupima, kutathmini, kuhakiki na kuchunguza mambo. Mapenzi yake kwa Muuza Madafu yanatokea tu mara anapomwona kwa mara ya kwanza. Suala la kwamba mapenzi huweza kutokea hivi si suala la mjadala – hufanyika na wanasaikolojia (miongoni mwa wataalamu wengine) wameeleza sababu lukuki za kwa nini hili hutendeka. Hata hivyo, katika ulimwengu wa kibunilizi wa riwaya hii, tukio hili linamgusa msomaji kwa kiwango chake cha uhamasishaji hali ambayo inaweza kutufanya tuhisi kuwa umotishaji wake kama mhusika unaishia kuwa wa 'nje-ya-matini' au,

kwa lugha ya Genette 'nje ya daigesia' kwa kuhusisha hatima yake na ile ya Aziza katika "Mke Wangu". Lakini kwa upande mwingine, labda hiki ni kielekezi kwenye upatanifu uliopo wa matendo ya mwanadamu.

3.3 Ulimwengu wa Kibunilizi, Suala la Mtazamo na Mwonoulimwengu

Mojawapo ya masuala muhimu ya kuchunguzwa katika uhakiki wa fasihi ni uundaji wa ulimwengu wa kibunilizi. Mwandishi anaposimulia kisa, kuwasawiri wahusika na kuyaonesha matendo yao hufanya hivi kwa kuwaweka kwenye muktadha fulani ambao tunaueleza kama ulimwengu wa kibunilizi. Kimsingi, suala la ulinganishaji wa ulimwengu wa kibunilizi wa hadithi fupi na ulimwengu wa kibunilizi wa riwaya lina changamoto kubwa (na labda kwa kiasi fulani linapotosha). Mawanda ya riwaya ni mapana mno na ulimwengu wake ni kama tunavyoona katika riwaya hii.

Hatuwezi kuangalia wala kuzungumzia ulimwengu wa kibunilizi wa kazi zinazohusika pasi na kuchunguza suala la utamaduni. Kimsingi, kazi hizi mbili ni za waandishi ambao wamekulia katika utamaduni unaofanana. Tofauti ya tanzu haitupi nafasi kubwa ya kulinganisha ulimwengu unaozungumziwa lakini inatupa ishara muhimu ambayo nitapenda kuiangalia hapa- muuza madafu. Mnazi (unaozaa madafu) una nafasi kubwa katika utamaduni wa waandishi, na kwa hivyo, ishara ya muuza madafu si ishara tu inayofungamanishwa na kitu ambacho ni muhimu katika jamii inayohusika, pia ni ishara inayokitwa kwenye 'roho' ya utamaduni wenyewe.

Hii ina maana kuwa kitendo cha Halima kumpenda na kutaka kujitambulisha na Muuza Madafu hakina maana tu katika kiwango cha kijuujuu - cha mwanamke anayempenda mwanamume wa ngazi ya chini, bali ni ishara ya kutotaka kuuasi msingi wa uhalisia wa maisha yake mwenyewe. Kuna jinsi fulani ambavyo kwa kumpenda Muuza Madafu, Halima anaishia kujipenda na kuipenda asili na kuwako kwake - kwa kiasi fulani kujikubali na kutovutiwa au kutekwa na hawaa na maisha, fuska na mali kunakohusishwa na mkondo wa maisha ya kisasa ambayo yanafungamanishwa na utandawazi.

Mapambano yanayotokea kati ya Halima na *Mwenye Meno* sio tu mapambano kati ya mwanamke na mwanamume anayeongozwa na tamaa (na labda hata uchuro) bali ni harakati ya kiitikadi baina ya historia na mabadiliko, uhafidhina na uanamapinduzi na mwanamke na mfumo mzima wa ubabedume. Kila mmoja anaishia kwenye msingi huu kuwa ishara ya tabaka mahususi. Halima anaisimulia upya hadithi au simulizi ya mwanamke na kwa jinsi hii kuipinga simulizi kuu inayotawala jamii inayodhibitiwa na mfumo wa ubabedume. Usemi wake, kwa hivyo, ni mlumbo/diskosi kinzani dhidi ya ubabedume. Muuza Madafu ni mwenzake kwa kuwa yeye (kama Halima na wanawake wenzake) amepambana na kuathirika kutokana na mfumo wa kukandamiza unaoongozwa na tabaka la 'Wenye Meno'. Hata hivyo, kama ilivyo kwenye msemo wa Kiswahili, 'kukaanga mbuyu kuwaachia wenye meno watafune', kizazi cha akina Halima (na tabaka

analowakilisha) kitaishia pia kuwa na ujasiri wa kukabili hayo magumu yanayosababishwa na tabaka la juu na hatimaye kuyatatua. Ung'amuzi wa ukweli huu ndiyo unaoashiriwa na ufumbuzi na mwisho wa riwaya hii ambapo Mwenye Meno anajiua na kuitoa mali yake kwa Halima aitumie kwa faida ya wengine.

Yamkini suala la mjadala linalobakia hapa ni kama mabadiliko yatakayotokea katika jamii yatategemea kani au nguvu za tabaka linalokandamizwa kutokana na alichokieleza Maksi kama ung'amuzi wa kitabaka au ung'amuzi wa kisaikolojia wa tabaka hilo linalodhalilisha. Katika riwaya ya *Wenye Meno*, Halima ni mhusika ambaye ana nafasi kubwa katika kuidengua misingi ya ujanadume iliyoimarishwa katika jamii na mfumo wa ubabedume. Kwa kiasi kikubwa, huyu ni mhusika wa kiumbuzi–anauumbua na kuupinga sio tu mfumo wenyewe, pia uhusika katika jamii ya aina hiyo. Hii ni sifa ambayo inamtenga kwa kiasi kikubwa na mhusika anayepatikana katika hadithi fupi ya M. S. Abdulla.

4.0 Hitimisho

Makala hii inabainisha namna tofauti ambavyo matini za kifasihi huhusiana, kuathiriana na kutagusana. Suala hili katika maandishi ya zamani lilichunguzwa kwa misingi ya dhana ya athari na kuathiriana. Wapo wananadharia wa mwingilianomatini ambao wanaamini kuwa uhusiano baina ya matini ni sifa isiyoweza kuepukika. Bakhtin anadahili kuwa kila kauli inayotamkwa huwa kimsingi inaijibu kauli iliyoitangulia na ambayo inahusiana nayo kusemezano. Genette naye anasema kuwa fasihi yoyote ile hupatikana katika ngazi ya pili, kwa kuwa kimsingi fasihi inaweza tu kutokana na fasihi nyingine. Kazi zilizochunguzwa hapa zinaelekea kuakisi ukweli huu kwa kiasi kikubwa—kwamba matini zinaingiliana, kuathiriana au hata kubomoana kwenye mwanda wa kimwingilianomatini. Hili ni suala ambalo kwa kiasi kikubwa linaweza kuchochea mjadala mkubwa kuhusu suala zima la ubunifu wa kazi au matini za kifasihi.

Mwingilianomatini ni sifa ambayo ipo kwenye fasihi na ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwako katika fasihi simulizi kwa miaka na dahari japo labda hatuiwazii sana kwenye uwanja huo kama ambavyo tunaishughulikia katika fasihi andishi. Ikiwa tutakubaliana kuwa lugha yenyewe ni 'ya kijamii' na kwa namna hii mwandishi hana lugha yake kama mtu au kiumbe binafsi basi inawezekana kudai kuwa fasihi nayo ina sifa hiyohiyo 'ya kijamii' na kwa hivyo suala la kuhusiana kwa matini si jambo geni wala halipaswi kushangaza au kuchochea mjadala. Kwa kiasi kikubwa, matini za kifasihi zinaingiliana, kuhusiana, kusemezana, kuathiriana, kukinzana na hata kudenguana katika mwanda wa kimwingilianomatini na kwa kiasi fulani basi inawezekana kukubaliana na Gerard Genette katika andiko lake la *Palimpsests*, kuwa 'fasihi inatokana na fasihi'. Katika muktadha huu, usemezano na mwingilianomatini uliopo kwenye

kazi zinazohusika hapa ni jambo la kuonewa fahari hasa kwa kuwa linatuelekeza kwenye jinsi ubunifu unavyoweza kuwa na sura nyingine.

Marejeleo

- Abdulla, M.S. (2007). "Mke Wangu" katika Ken Walibora na Said A. Mohamed *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Moran Publishers. Kur. 17-25
- Bloom, H. (1975). *The Anxiety of Influence. A Theory of Poetry*. Oxford/New York: Oxford University Press.
- Flaubert, G. (1991). *Madame Bovary*. New York: Quality Paperback Book Club.
- Genette, G. (1997a). *Paratexts. Thresholds of Interpretation*. Cambridge: Cambridge University Press.
- _____ (1997b). *Palimpsests. Literature in the Second Degree*. London: University of Nebraska Press.
- Hussein, E. (1973). *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press.
- Llosa, M.V. (2007). *The Bad Girl. Edith Crossman (Trans)*. London: Faber and Faber Ltd.
- Mbogo, E. (1980). *Giza Limeingia*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mohamed, S.A. (2016). *Mashetani Wamerudi*. Nairobi: Spotlight Publishers Ltd.
- _____ (2018) *Wenye Meno*. Nairobi: Spotlight Publishers Ltd.
- Msokile, M. (1990). *Usiku Utakapokwisha*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Wamitila, K.W. "Kanzi ya Fasihi 3: Misingi, Nadharia za Uhakiki na Tahakiki". (Mswada wa kitabu, utachapishwa 2025).